

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Anuaniyasimu "ELIMU"  
Simu: 026 296 35 33  
Baruapepe: info@moe.go.tz  
Tovuti: [www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz)



Mji wa Serikali,  
Eneo la Mtumba,  
Mtaa wa Afya,  
S. L. P. 10,  
40479 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

22 Juni, 2020

**TAMKO LA SERIKALI KUHUSU KUFUNGULIWA KWA SHULE NA VYUO**

Ndugu Wananchi, kama mnavyofahamu, jana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alitoa maelekezo ya kuanza kwa shughuli mbalimbali ambazo zilisimamishwa ili kuzuia kusambaa kwa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (COVID-19). Katika maelekezo yake Mheshimiwa Rais, pamoja na mambo mengine, aliagiza vyuo vifunguliwe na pia wanafunzi wa Kidato cha Sita warejee shuleni kuanzia tarehe 01 Juni, 2020.

Kufuatia maelekezo hayo ya Mheshimiwa Rais, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inapenda kutoa utaratibu wa utekelezaji kama ifuatavyo:

**Wanafunzi wa Kidato cha Sita**

Wizara inazielekeza Shule zote zenye Wanafunzi wa Kidato cha Sita kuanza maandalizi mapema ili wanafunzi waweze kupokelewa na kuanza masomo rasmi tarehe 01 Juni 2020. Hii ina maana kuwa Shule za Bweni ziwe tayari kuwapokea wanafunzi kuanzia siku ya Jumamosi, tarehe **30 Mei, 2020**. Shule za kutwa nazo zinaelekezwa kufanya maandalizi stahiki ili masomo yaanze rasmi tarehe **01 Juni, 2020**. Ikumbukwe kwamba ufunguzi huu wa shule unahusu wanafunzi wa Kidato cha Sita pekee, hautawahusu wanafunzi wa vidato vingine.

## **Mtihani wa Kidato cha Sita**

Wanafunzi wa Kidato cha Sita wataendelea na masomo ambayo yatahitimishwa kwa kufanya Mtihani wao wa mwisho. Mtihani wa Kidato cha Sita utanza rasmi tarehe **29 Juni, 2020** na kukamilika tarehe **16 Julai, 2020**. Mtihani huo utafanyika sambamba na mitihani ya Ualimu.

Tunatarajia kuwa Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) litatoa matokeo ya mitihani hiyo kabla ya tarehe **31 Agosti, 2020** ili wanafunzi hao wawe na muda wa kuomba udahili katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Kwa ratiba hii wanafunzi wataweza kujiunga na Vyuo vya Elimu ya Juu katika muda muafaka bila kuathiri ratiba ya masomo kwa mwaka 2020/2021.

## **Wanafunzi wa Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu**

Kwa upande wa Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu, Wizara inaelekeza navyo vianze maandalizi ili viweze kupokea wanafunzi kuanzia tarehe **01 Juni 2020**. Nazielekeza mamlaka za vyuo hivyo, kwa maana ya Mabaraza na Seneti kupanga ratiba za masomo kwa lengo la kufidia muda ambao wanafunzi walikuwa nyumbani na vyuo vyote vitapaswa kuwasilisha ratiba zao kwa mamlaka husika yaani Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ili mwaka huu wa masomo ukamilike kwa wakati muafaka bila kuathiri ratiba za masomo ya mwaka 2020/2021.

## **Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

Wizara inapenda kuwahakikishia wanafunzi na Vyuo vya Elimu ya Juu kuwa Serikali ilishatoa jumla ya **Shilingi Bilioni 122.8** ambapo **Shilingi Bilioni 63.7** ni kwa ajili ya chakula na malazi; na **Shilingi Bilioni 59.1** ni ada za wanafunzi. Hivyo nazielekeza mamlaka za Vyuo Vikuu kuhakikisha kuwa **nyaraka zote muhimu** zinazohitajika ili kupokea fedha toka Bodi ya Mikopo zinaandaliwa na kuwasilishwa kabla ya tarehe **28/5/2020**. Hii itawezesha Bodi ya Mikopo kutuma fedha kwa wakati muafaka kabla wanafunzi hawajafika vyuoni. Aidha naelekeza pia Vyuo Vikuu viweke maofisa wa kutosha kwenye eneo la ugawaji wa mikopo kwa wanafunzi ili wanufaika wapate fedha zao mapema na kuwawezesha kusoma kwa utulivu ikizingatiwa watapaswa kuwa madarasani kwa muda mrefu zaidi ili kufidia siku.

Kwa upande mwingine Serikali inaviagiza Vyuo Vikuu vyote kuwasilisha Bodi ya Mikopo nyaraka zao za maombi ya malipo ya ada za wanafunzi (yaani tuition fees) ili malipo hayo yaweze yafanyike mapema ili shughuli za utawala katika vyuo ziweze kuendelea bila pingamizi lolote.

### **Tahadhari kuhusu Virusi vya Corona**

Wizara inapenda kuelekeza shule zote zenye Wanafunzi wa Kidato cha Sita na Vyuo vyote vitakavyofunguliwa kuanzia tarehe **01/06/2020** kuhakikisha wanazingatia maelekezo yote kuhusu kujikinga na Virusi vya Corona. Shule pamoja na Vyuo vinapaswa kuandaa vifaa vya kunawia mikono kwenye maeneo muhimu kama vile madarasa, kumbi za mikutano na mabwalo ya chakula.

### **Hitimisho**

Wizara inapenda kutoa wito kwa walimu pamoja na wanafunzi kuhakikisha wanajituma katika masomo yao ili waweze kukamilisha mihtasari kwa wakati bila kuathiri mwaka wa masomo 2020/2021.

Imetolewa na:



Mhe. Prof. Joyce Ndalichako (Mb.)  
**Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia**